

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE

MKOA WA NJOMBE

Simu: 026-2968833

Faksi: 026- 298832

**E- mail: td@njombetowncounci.go.tz
njombetc@gmail.com**



**S.L.P 577,
NJOMBE.**

Tovuti: www.njombetowncouncil.go.tz

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UZINDUZI WA SIKU YA MAZOEZI
KIMKOA.

Kufuatia agizo la Mheshimiwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu kuwataka Wananchi kote nchini kutumia jumamosi ya pili ya mwezi kushiriki katika mazoezi, Halmashauri ya Mji Njombe itakua mwenyeji wa Uzinduzi wa siku ya Mazoezi Kimkoa yatakayofanyika siku ya jumamosi ya tarehe 11/03/2017 katika Viwanja vya magereza vilivyopo katika mtaa wa Kambarage.

Uzinduzi huo unatarajiwa kuanza na zoezi la mchakamchaka kuanzia geti la Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kuelekea uwanja wa magereza na mgeni rasmi katika uzinduzi huo anatarajiwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe **Mh. Christopher Ole Sendeka.**

Wananchi wote na watumishi wa Serikali na Taasisi zote za Mkoa wa Njombe mnatakiwa kushiriki bila kukosa mkiwa mmevaa sare za michezo saa kumi na mbili kamili asubuhi eneo la makutano ambapo ni geti la Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

TOKOMEZA MAGONJWA YANAYOEPUKIKA KATIKA MKOA WA NJOMBE KWA KUSHIRIKI KATIKA MAZOEZI.

Imetolewa na,

**Hyasinta Kissima,
Afisa Habari- Halmashauri ya Mji Njombe.**